



## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUSITISHWA KWA LESENI ZA USAFIRISHAJI ABIRIA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inautaarifu umma kuwa imesitisha leseni za usafirishaji abiria kwa mabasi 22 kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Februari, 2023.

Hatua hii ni kutokana na vitendo vya kuingilia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kusababisha mfumo kutotuma taarifa ama kutuma taarifa kwa kurukaruka (skipping). Hapa kuna baadhi ya mabasi ambayo baada ya wataalamu wa Mamlaka kufanya uchunguzi, waligundua betri za vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTDs) zimeharibiwa na mfumo wa umeme kubadilishwa.

Kitendo cha kuingilia Mfumo wa VTS ni ukiukwaji wa Kanuni ya 51 ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020. Hivyo, Mamlaka imechukua hatua ya kusitisha leseni hizo kwa mujibu wa Sheria ya LATRA ya Mwaka 2019 na Kanuni zake za mwaka 2020. Kabla ya kurejeshewa leseni zao, watoa huduma wa mabasi husika walitakiwa kuwafikisha Jeshi la Polisi madereva wa mabasi husika ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168.

Wakati huohuo Mamlaka imewaandikia barua watoa huduma ambao vifaa vya kufuatilia mwenendo wa magari yao (VTDs) vinaonyesha viasharia vya kuchezeza na kuwataka watoe maelezo ya kwanini leseni zao zisisitishwe kutokana na kasoro hizo. Uchunguzi wa magari hayo bado unaendelea na pale itakapothibitika kuwa kuna uvunjaji wa kanuni leseni za magari husika zitasitishwa.

Mamlaka inawatahadharisha wamiliki wa mabasi na madereva wao kuzingatia Kanuni za Leseni za Usafirishaji (mabasi ya abiria) za Mwaka 2020 na Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 kwa kuongeza usimamizi wa huduma.

Katika hatua nyingine Mamlaka imeendelea kutekeleza jukumu la usajili wa madereva wa vyombo vya moto kibiashara kwa mujibu wa kifungu Na 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413. Jumla ya madereva 13,180 wameshasajiliwa kwenye mfumo wetu na kati yao madereva 840 wameshafanya mitihani kwa ajili ya kuthibitishwa.

Kutokana na takwa hilo la kisheria, Mamlaka inawaagiza wamiliki wote wa magari yanayotoa huduma kibiashara kuhakikisha madereva wao wote wamesajiliwa ifikapo tarehe 30 Aprili, 2023. Usajili unafanyika kwenye ofisi zote za LATRA Tanzania Bara na hivyo madereva wote waelekezwe kufika kwenye ofisi za LATRA ili waweze kusajiliwa.

Kwa madereva watakaoshindwa kufika kwenye ofisi za LATRA wanaweza kutuma maombi ya kusajiliwa kupitia anuani ya <https://rrims.latra.go.tz/login>.

Maombi ya kusajiliwa yaambatishwe **Leseni ya udereva, Cheti cha taaluma ya udereva kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali na Taarifa ya Uthibitisho wa afya kutoka Hospitali ya Serikali**. Fomu ya Uthibitisho wa Afya inapatikana kwenye tovuti [www.latra.go.tz](http://www.latra.go.tz) na ofisi za LATRA.

### Jedwali 1. Orodha ya Mabasi Yaliyositishiwa Leseni.

Na.	Basi	Mmiliki	Tarehe ya Leseni Kusitishwa
1.	T366DME	Kapesa Benedict Mberesero	19.1.2023
2.	T708DPS	Jacob Deka Malesa	19.1.2023
3.	T836DWU	Dar Express (Yudika Eliya Mremi)	10.2.2023
4.	T586AJH	Ahmad Luxury Coach	13.2.2023
5.	T348DFS	Kidia One	14.2.2023
6.	T454DHP	Luwinzo Express (Seif Omary Luwinzo)	14.2.2023
7.	T166DQX	Maning Nice Company Limited	14.2.2023

8.	T274DCP	Jumanne Mohammed Khamis	15.2.2023
9.	T376CAX	NBS Classic Co. Ltd	15.2.2023
10.	T114DRZ	NBS Classic Co. Ltd	15.2.2023
11.	T471 DLZ	NBS Classic Co. Ltd	15.2.2023
12.	T842DQV	Super Feo Express (Omary Marcus Msigwa)	15.2.2023
13.	T835CQQ	Mlalo Express (Ibrahim Issa Kimweri)	15.2.2023
14.	T417CTS	Paulo Malekana Magadula	15.2.2023
15.	T131DRE	George Benedict Temba	15.2.2023
16.	T447CHQ	Simba Video (Thabit Said Omary)	15.2.2023
17.	T843DLX	Super Feo Express	15.2.2023
18.	T616BBQ	Kimotco Intertrade Co. Limited	15.2.2023
19.	T567DFA	Frester Investment	15.2.2023
20.	T751DTB	Huruma Enock Mahenge	15.2.2023
21.	T994DQT	Tashriff Trans	15.2.2023
22.	T339DCR	Ally Soud Ally	15.2.2023

**Imetolewa na:**  
Mkurugenzi Mkuu  
Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini  
21 Februari, 2023